**BARAZA LA WAWAKILISHI – ZANZIBAR**

**ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO**

**BARAZA LA KUMI LA WAWAKILISHI**

**MKUTANO WA TATU**

**Kikao cha Kumi – Tarehe 19 Mei, 2021.**
Kikao Kitaanza Saa 3.00 (Tatu) Asubuhi
na Dua itasomwa.

## I. HATI ZA KUWASILISHA MEZANI:

### Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi:

Hotuba ya Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi kwa Mwaka 2021/2022.

### Mwenyekiti wa Kamati ya Mawasiliano, Ardhi na Nishati:

Hotuba ya Maoni ya Kamati ya Mawasiliano, Ardhi na Nishati kuhusu Hotuba ya Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi kwa Mwaka 2021/2022.

**II. <u>MASWALI:</u>**

## Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi na Utawala Bora:

75. MHESHIMIWA MACHANO OTHMAN SAID (Jimbo la Mfenesini) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi na Utawala Bora:

Katika kukabiliana na wimbi la uhalifu pia kupunguza mrundikano wa wafungwa (wanafunzi) katika vyuo vyetu vya mafunzo, Serikali imepitisha Sheria ya baadhi ya wafungwa wenye vifungo vidogo kwenda kuitumikia jamii katika muda wao wote wa kifungo. Hata hivyo, pamoja na kuwepo kwa Sheria hiyo kwa muda mrefu bado haijaanza kufanya kazi hadi hivi sasa.

(a) Kwa kuwa lengo la Serikali halikufanikiwa na kwa kuwa hakuna juhudi zozote za kuanza utaratibu huo, Je, Serikali inasemaje kuhusu jambo hilo.

(b) Je, ni sababu gani hasa za msingi zilizopelekea Sheria hiyo ishindwe kufanya kazi.

## Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ:

40. MHESHIMIWA KOMBO MWINYI SHEHE (Jimbo la Wingwi) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ:

Katika eneo la Kwapweza Kijichame ndani ya Shehia ya Sizini kimejengwa kituo cha Zimamoto cha Wilaya ya Micheweni. Wakati kituo hicho kilipotaka kujengwa wakulima waliokuwa wanalitumia eneo hilo waliahidiwa kulipwa fidia pamoja na usumbufu wa kukosa kulitumia tena eneo hilo.

Je, ni lini Serikali itaitekeleza ahadi hiyo iliyotolewa kwa wakulima hao.

**Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango**

95. MHESHIMIWA HAJI SHAABAN WAZIRI (Jimbo la Uzini) Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango:

Je, kuna mpango gani wa wanachama wa ZSSF kufaidika na gawio la nyongeza ya pesa zinazopatikana katika faida inayopatikana kutoka kwenye miradi inayofanyika.

**Wizara ya Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo:**

34. MHESHIMIWA SHAMATA SHAAME KHAMIS (Jimbo la Micheweni) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo:

Uzoefu unaonesha kuwa wananchi wa Zanzibar wamekuwa na kawaida ya kuagiza mifugo kutoka Tanzania Bara na kuiingiza kupitia bandari zinazotambulika na Serikali zikiwemo Kisakasaka, Muwanda, Wesha, Wete na nyenginezo.

(a) Je, ni idadi gani ya mifugo imeingizwa hapa nchini kwa kipindi cha mwezi wa Julai 2020 mpaka Aprili, 2021.

(b) Je, ni kiasi gani cha fedha Serikali imekusanya kupitia biashara hii ya uingizaji wa mifugo.

(c) Je, Wizara inatumia mbinu gani madhubuti kuhakikisha mapato yatokanayo na uingizaji wa mifugo hayapotei.

**Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi:**

64. MHESHIMIWA MACHANO OTHMAN SAID (Jimbo la Mfenesini) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi:

Naipongeza Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa ujenzi wa barabara ya kisasa ya Mkokotoni hadi Bububu Polisi. Hata hivyo, baada ya ujenzi huo wananchi wa eneo la Mfenesini na Kama njia ya Bumbwini wamekuwa wakipata madhara ya mafuriko kila inaponyesha mvua kubwa jambo ambalo linasababisha hasara kubwa na majonzi kwa wananchi hao. Kwa kuwa mafuriko hayo huwa yanashuhudiwa hata na viongozi wa kitaifa.

Je, Serikali ina mpango gani wa kuwaondolea wananchi tatizo hilo.

**Wizara ya Biashara na Maendeleo ya Viwanda:**

124. MHESHIMIWA HABIB ALI MOHAMED (Jimbo la Mtambwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Biashara na Maendeleo ya Viwanda:

Tunao vijana ambao walipata mafunzo mazuri ya ujasiriamali kutoka Chuo Kikuu cha Dar-es-Salaam lakini wameshindwa kuitumia elimu yao kujikwamua kiuchumi kutokana na ukosefu wa fedha na vifaa.

(a) Je, Wizara ina mpango gani ya kuwawezesha vijana hawa ili elimu yao ilete tija iliyokusudiwa.

(b) Ni ipi nafasi ya wawekezaji wadogo wadogo nchini mwetu katika vipaumbele vya Serikali.

**Wizara ya Maji, Nishati na Madini:**

113. MHESHIMIWA YUSSUF HASSAN IDDI (Jimbo la Fuoni) -

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maji, Nishati na Madini.

Kwa muda mrefu sasa kisima cha Ras-Al-Khaimah kilichopo Fuoni Birikani hakijakamilika na kupelekea wananchi wa maeneo hayo kukosa huduma ya maji safi na salama.

Je, ni lini kisima hicho kitakamilika.

**Wizara ya Afya, Ustawi wa Jamii, Wazee, Jinsia na Watoto:**

18. MHESHIMIWA HASSAN HAMAD OMAR (Jimbo la Kojani) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Afya, Ustawi wa Jamii, Wazee, Jinsia na Watoto:

Maradhi ya kichocho ni moja kati ya magonjwa yanayosumbua sana hususan katika maeneo mbali mbali ya vijijini. Kwa kuwa athari zake ni mbaya kuanzia utotoni hadi katika umri wa utu uzima, na ikizingatiwa kuwa wataalamu wanatueleza kwamba bila kowa (snail) hakuna kichocho.

Je, ni njia gani za kitaalamu zitakazotumika vijijini kwetu ili kuondosha kowa "snail' na hatimae tuweze kuepukana na kichocho.

## III. HOJA ZA SERIKALI:

### Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi:

Kwamba Baraza hili lijadili Makusudio na Shabaha zilizomo katika Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi kwa mwaka 2021/2022.

| | |
|---|---|
| **Zanzibar,** | **(Raya Issa Msellem)** |
| **19 Mei, 2021.** | **KATIBU WA BARAZA** |